ELIMU

# ADEM: Taasisi inayojenga viongozi wa Elimu kwa Tanzania ya kesho

## Uongozi Bora wa Elimu ni Msingi wa Mafanikio ya Taifa


Mafunzo ya Uongozi na Usimamizi Fanisi wa Shule pamoja na Utawala bora wa Elimu kwa maafisa elimu kata, mafunzo haya yanatolewa na ADEM kwa kushirikiana na African Centre for School Leadership (ACSL) kupitia VVOB kwa kufadhiliwa na Mastercard Foundation.

**Na Mwandishi Wetu**

Katika juhudi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania za kuendelea kuboresha ubora wa elimu na kuandaa rasilimali watu yenye uwezo wa kushindana katika uchumi wa kisasa, suala la uongozi na usimamizi wa elimu limeendelea kupewa kipaumbele kikubwa.

Wataalamu wa elimu wanakubaliana kwamba mafanikio ya shule na taasisi za elimu hayategemei tu walimu na miundombinu bora, bali pia viongozi wenye uwezo wa kusimamia rasilimali, kuhamasisha ubunifu na kuhakikisha sera za elimu zinatekelezwa kwa ufanisi.

Ni katika muktadha huo ambapo Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM) umeendelea kuwa taasisi muhimu katika kuandaa viongozi wa elimu wenye maarifa, ujuzi na maadili yanayohitajika katika karne ya 21.

ADEM ni taasisi ya Serikali iliyo chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye jukumu la kuendeleza uongozi, usimamizi na utawala katika sekta ya elimu nchini. Tangu kuanzishwa kwake, taasisi hii imekuwa ikitoa mafunzo kwa viongozi wa elimu katika ngazi mbalimbali kwa lengo la kuimarisha ubora wa huduma za elimu nchini.

**Historia ya ADEM**

Asili ya ADEM inaanzia mwaka 1978 kupitia programu ya Management Training for Educational Personnel (MANTEP Institute) iliyokuwa ikitoa mafunzo ya Uongozi na Utawala kwa viongozi wa Elimu nchini. Kutokana na umuhimu wa programu hiyo na mahitaji yanayoongezeka ya viongozi wenye ujuzi wa usimamizi, Serikali ilianzisha rasmi Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM) chini ya Sheria ya Bunge Sura 245 ya uanzishwaji wa Wakala za Serikali.

Leo hii, ADEM imekua na kuwa taasisi maalumu inayotoa mafunzo, kufanya tafiti na kutoa ushauri elekezi katika masuala ya uongozi na usimamizi wa Elimu pamoja na Uthibiti Ubora wa Shule. Makao makuu yake yapo Bagamoyo, Mkoa wa Pwani, huku ikiwa na kampasi katika mikoa ya Mwanza na Mbeya ili kusogeza huduma karibu zaidi na wadau wa elimu nchini.

**Kukuza Uwezo wa Viongozi wa Elimu**

Katika miaka ya hivi karibuni, sekta ya elimu imepitia mabadiliko makubwa yanayohitaji viongozi wenye uwezo wa kufanya maamuzi sahihi katika mazingira yenye changamoto mbalimbali.


Mtendaji Mkuu wa ADEM, Dkt. Maulid J. Maulid akifungua Mafunzo ya Uongozi wa Kimkakati yanayoendelea nchini.

ADEM imekuwa mstari wa mbele kuwajengea uwezo wakuu wa shule, walimu wakuu, maafisa elimu wa kata, halmashauri na mikoa, wathibiti ubora wa shule, wakufunzi wa vyuo vya ualimu pamoja na wasimamizi wengine wa elimu.

Mafunzo yanayotolewa yanajikita katika maeneo muhimu kama vile: -uongozi wa taasisi za elimu, usimamizi wa rasilimali watu, usimamizi wa fedha, mipango ya maendeleo ya shule, ufuatiliaji na tathmini, uongozi wa mabadiliko, matumizi ya TEHAMA katika usimamizi wa elimu na vilevile uthibiti ubora wa shule.

Kupitia mafunzo haya, viongozi wa elimu wanapata uwezo wa kusimamia taasisi zao kwa ufanisi zaidi na kuongeza uwajibikaji katika maeneo yao ya kazi.

Programu Zinazotoa Suluhisho kwa Mahitaji ya Sasa

Katika kukabiliana na mahitaji mapya ya sekta ya elimu, ADEM imeendelea kuboresha programu zake za mafunzo.

**Miongoni mwa programu zinazotolewa ni:**

- Stashahada ya Uongozi, Usimamizi na Utawala katika Elimu;
- Stashahada ya Uthibiti Ubora wa Shule;
- Stashahada ya TEHAMA na Usimamizi wa Elimu;
- Stashahada ya Usimamizi wa Elimu Jumuishi;
- Stashahada ya Usimamizi wa Elimu ya Amali;
- Mafunzo endelevu kwa viongozi wa elimu;
- Mafunzo ya muda mfupi kulingana na mahitaji ya taasisi mbalimbali.

Programu hizi zimekuwa zikiwasaidia viongozi wa elimu kuendana na mabadiliko ya sera, teknolojia na mbinu mpya za usimamizi wa taasisi za elimu.

**Mapinduzi ya Kidijitali katika Mafunzo**

Katika zama za teknolojia, ADEM imewekeza kwa kiwango kikubwa katika mifumo ya kidijitali ili kuboresha utoaji wa mafunzo.

Taasisi imeanzisha mifumo inayowezesha wanafunzi kufanya usajili, kupata taarifa za kitaaluma, kufuatilia maendeleo yao na kushiriki mafunzo kwa njia ya mtandao.

Mfumo wa "blended learning" unaochanganya mafunzo ya ana kwa ana na yale ya mtandaoni umeongeza upatikanaji wa elimu kwa viongozi wa elimu waliopo katika maeneo mbalimbali ya nchi bila kuathiri majukumu yao ya kazi.

Hatua hii imeifanya ADEM kuwa miongoni mwa taasisi za mafunzo zinazokwenda sambamba na maendeleo ya teknolojia duniani.

**Mchango Katika Mageuzi ya Elimu Tanzania**

Kwa mujibu wa wadau mbalimbali wa elimu, mchango wa ADEM unaonekana moja kwa moja katika kuimarika kwa usimamizi wa shule na taasisi za elimu nchini.

Wahitimu wa ADEM wamekuwa wakichangia kuongeza uwajibikaji katika taasisi za elimu, kuboresha matumizi ya rasilimali za umma, kuimarisha usimamizi wa walimu na wanafunzi, kuboresha mazingira ya kujifunzia, kuongeza ufaulu na ubora wa matokeo ya wanafunzi na kuimarisha utekelezaji wa sera za elimu.

"Kwa kiasi kikubwa, viongozi wengi wa elimu waliopitia mafunzo ya ADEM wamekuwa sehemu ya mabadiliko chanya yanayoonekana katika shule na taasisi mbalimbali nchini" anasema Mtendaji Mkuu wa ADEM, Dkt. Maulid J. Maulid.

**Mikakati ya ADEM kwa Mwaka 2026**

Akielezea mikakati ya ADEM kwa mwaka 2026, Dkt Maulid alisema kuwa ni sehemu ya kuendelea kuboresha huduma zake, ADEM imeweka mikakati mbalimbali kwa mwaka 2026 ambapo miongoni mwa mikakati hiyo ni pamoja na kuboresha mitaala ili iendane na mahitaji ya sasa, kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji, kupanua mafunzo ya mtandaoni, kuongeza ushirikiano wa kimataifa, kuimarisha tafiti za kielimu, kuwajengea uwezo wakufunzi katika mbinu mpya za ufundishaji na kupanua huduma za mafunzo katika kanda mbalimbali nchini.

**Changamoto na Mwelekeo wa Baadaye**

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana, ADEM bado inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo mahitaji makubwa ya mafunzo, upanuzi wa miundombinu, kuongezeka kwa matumizi ya teknolojia na mahitaji ya rasilimali kwa ajili ya tafiti.

Hata hivyo, taasisi inaendelea kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Ofisi ya W

Inaendelea Uk 12



Mtendaji Mkuu wa ADEM, akizungumza na Ndg Dedan Rutazika, Kaimu Afisa Elimu Mkoa wa Shinyanga, wakati alipoenda kufanya Ufunguzi wa Mafunzo ya Uongozi wa Kimkakati kwa Mkoa wa Shinyanga yanayoendelea nchini.

Inatoka Uk 11

aziri Mkuu-TAMISEMI, mashirika ya maendeleo na wadau wengine wa elimu ili kuhakikisha changamoto hizo zinapatiwa ufumbuzi endelevu.

"Maendeleo ya elimu bora hayawezi kupatikana bila viongozi wenye uwezo wa kusimamia taasisi za elimu kwa ufanisi. ADEM itaendelea kuwa kitovu cha kuandaa viongozi wa elimu watakaoweza kuleta mabadiliko chanya katika Taifa." Aliongeza Dkt Maulid.

**KISANDUKU MAALUM KWA UFUPI KUHUSU ADEM**

**Makao Makuu:** Bagamoyo, Mkoa wa Pwani

**Kampasi:** Bagamoyo, Mwanza na Mbeya

**Ilikotokana:** Programu ya MANTEP (1978)

**Jukumu Kuu:** Kuendeleza uongozi, usimamizi na utawala katika elimu

**Walengwa:** Wakuu wa shule, walimu wakuu, maafisa elimu, wathibiti ubora wa shule na viongozi wengine wa elimu

**Huduma:** Mafunzo, tafiti na ushauri elekezi

**Mfumo wa Mafunzo:** Ana kwa ana, mtandaoni na blended learning.

**Ushirikiano wa Kimkakati Unaokuza Ubora wa Elimu**

Katika kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, ADEM imeendelea kujenga ushirikiano na taasisi mbalimbali za Serikali, vyuo vikuu, mashirika ya maendeleo na wadau wa elimu ndani na nje ya Tanzania. Ushirikiano huu umekuwa muhimu katika kuboresha mafunzo, kufanya tafiti, kuendeleza matumizi ya teknolojia na kuimarisha uwezo wa viongozi wa elimu nchini.

**Miongoni mwa washirika wakuu wa ADEM ni:**

Washirika wa Ndani ya Tanzania ADEM imekuwa ikishirikiana na wadau wa elimu mbalimbali ndani na nje ya nchi katika shughuli zake ikiwemo Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ikiwa ni mshirika mkuu mkuu katika kuandaa na kutekeleza sera pamoja na programu za mafunzo ya viongozi wa elimu.

Aidha, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) imekuwa mshirika mkubwa pia kwa kushirikiana katika mafunzo ya maafisa elimu, wakuu wa shule na viongozi wa elimu katika mamlaka za serikali za mitaa.

Taasisi zingine ni kama Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) katika masuala ya maendeleona utekelezaji wa mitaala na ubora wa elimu, Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA) katika maeneo ya tathmini na maboresho ya elimu.

Washirika wengine wa ndani ni pamoja na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) katika uthibiti wa ubora wa programu za mafunzo, Open University of Tanzania - kupitia makubaliano ya ushirikiano yanayolenga kuimarisha uongozi wa elimu, mafunzo ya walimu na tafiti za pamoja na Project Zawadi na Chuo cha Ukutubi na Utunzaji Nyaraka-SLADS - kushirikiana katika mafunzo ya muda mfupi ya uongozi na usimamizi wa elimu.

## Historia ya ADEM

**Asili ya ADEM inaanzia mwaka 1978 kupitia programu ya Management Training for Educational Personnel (MANTEP Institute) iliyokuwa ikitoa mafunzo ya Uongozi na Utawala kwa viongozi wa Elimu nchini. Kutokana na umuhimu wa programu hiyo na mahitaji yanayoongezeka ya viongozi wenye ujuzi wa usimamizi, Serikali ilianzisha rasmi Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM) chini ya Sheria ya Bunge Sura 245 ya uanzishwaji wa Wakala za Serikali.**

Katika kuonyesha ADEM inakuwa imara katika ushirikiano, pia imekuwa na washirika wa Kimataifa kama Shirika la kimataifa la maendeleo ya elimu (VVOB) linaloshirikiana na ADEM kuimarisha uongozi wa shule za sekondari Tanzania kupitia mafunzo ya kisasa ya blended learning, African Centre for School Leadership (ACSL) inashirikiana na ADEM katika kuboresha uongozi wa shule barani Afrika kupitia mafunzo ya muda mfupi.

Dkt Maulid ameongeza kuwa wadau wengine wa kimataifa wa nje ni Association for the Development of Education in Africa (ADEA) ambaye ni mshirika katika programu za kuendeleza uongozi wa elimu na kubadilishana uzoefu wa kitaaluma.

Aliongeza kuwa Education Sub-Saharan Africa (ESSA) ni mmoja ya mshirika katika miradi ya kuboresha matokeo ya kujifunza na usimamizi wa shule kwa ADEM kwa njia ya kufanya tafiti.

Wengine ni Forum for African Women Educationalists (FAWE) ambaye ni mshirika wa ADEM katika mipango ya uongozi wa elimu na usawa wa kijinsia katika elimu na vilevile Mastercard Foundation katika programu za maendeleo ya viongozi wa elimu na ubora wa ujifunzaji.


**Matokeo ya Ushirikiano Huo**

Dkt Maulid amezitaja faida na matokeo ya ushirikiano huo kuwa ADEM imeweza kupanua wigo wa mafunzo kwa viongozi wa elimu nchini, kuanzisha na kuimarisha mafunzo ya mtandaoni na blended learning, kuongeza fursa za tafiti na ubadilishanaji wa uzoefu wa kimataifa, kuimarisha ubora wa uongozi wa shule na taasisi za elimu nad kuchangia utekelezaji wa mageuzi ya elimu yanayoendelea nchini Tanzania.

**Wito kwa Wataalamu wa Elimu**

ADEM inawahimiza walimu, wakuu wa shule, maafisa elimu na wataalamu wengine wa sekta ya elimu kutumia fursa zilizopo za mafunzo ili kujiendeleza kitaaluma na kuongeza uwezo wao wa kiuongozi.

Kadri dunia inavyoendelea kubadilika kwa kasi, ndivyo mahitaji ya viongozi wa elimu wenye ubunifu, weledi na uwezo wa kutumia teknolojia yanavyozidi kuongezeka. Kupitia ADEM, Tanzania inaendelea kujenga kizazi cha viongozi wa elimu kitakachosaidia kuleta maendeleo endelevu ya Taifa kupitia elimu bora kwa wote.



Washiriki wa Mafunzo ya Uongozi na Usimamizi Fanisi wa Shule pamoja na Utawala Bora wa Elimu wakiwa kwenye eneo la mafunzo mkoani shinyanga, mafunzo haya yalikuwa chini ya ufadhili wa mradi wa Boost.